# KPSEA 2023 EXAMINER FINAL PREDICTION

# KISWAHILI MUDA: Saa 1 dak 40

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chaguajibu lako ionyeshe katika KARATASIYAMAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTTIMIÁ KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida. 5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatsi ya majibu.

**NAMBARIYAKO YA MTIHANI JINA**

**LAKO JINA LA SHULE SHULE**

**YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba ako kamili ya mtihani yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwamwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku,,
8. Iweke safi karatasi yako ya maibu.
9. Kwakila swali 1-30 umepewamajibu manne. Majibu'ha o yameonyeshwakwä herufi A, B,D naD. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilisi
10. Kwenye karatasi ya majibu,jibu sahihi lionyeshwe kwakuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilojibu.
11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwakila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku ulivyopewa.

## ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Hapo zamani za kale, katika ulimwengu wa wanyama, paliishi Swara na **Mbweha Swara na Mbweha walipendana kama chanda na pete.** Wawili hao walikuwa na familia zao. Kila mmoja alikuwa na nyumba yake, mke pamoja na watoto. Mbweha alikuwa na watoto sita naye Swara alikuwa na watoto watano. Marafiki hao **walifanya mambo yao kwa ushirikiano mkubwa**. Walifuga wanyama kama

vile mbuzi, ng'ombe, kondoo na ngamia. Wanyama hao waliwapa faida ya maziwa na wakati fulani kuwafanyia kazi.

Tofauti kubwa iliyokuwapo ni kuwa Swara alipenda shughuli za kilimo naye Mbweha alipenda sana ufugaji. Swara alipouza maziwa yake, alipanda miche kisha akaamua kuwekeza katika kilimobiashara. Alipanda mimea kama vile michungwa, mihindi, mitufaha na mingine. Alipovuna mazao ya mimea hiyo, alitoa gharama ya ukulima huo kisha akabaki na faida kubwa mno. Kwa kuwa kazi ilikuwa nyingi shambani, aliamua kuwapa wanyama wengine ajira. Kila alipovuna mazao yake, aliyauza na kuweka pesa alizozipata katika benki. Hiyo ilikuwa njia ya kuhakikisha kuwa pesa zake zisingeibwa na wahalifu. Uzalendo wa Swara ulijulikana sana alipolipa ushuru kutokana na mapato.

Kwa sasa, marafiki hao wawili ni matajiri wakubwa. Wakazi katika eneo hilo wanapenda sana kilimo, ufugaji na biashara. Vilevile, wao hulipa ushuru wa mapato mara kwa mara. Wamejifunza kwa Swara na Mbweha kuwa kulipa ushuru kuna manufaa makubwa katika nchi.

1. Ukirejelea maisha ya Swara, ni jambo gani lililokuwa la mwisho kati ya mambo haya?
    A. kulipa ushuru
    B. kuuza mazao ya shambani
    C. kufuga wanyama
    D. kuanzisha kilimo
2. Maneno **'walifanya mambo yao kwa ushirikiano mkubwa'** yanaonyesha kuwa Swara na rafiki yake walizingatia methali gani? A. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
    B. Majuto ni mjukuu huja baadaye.
    C. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.
    D. Panya wengi hawachimbi shimo.
3. Ni kweli kuwa kama Swara asingekuwa na mifugo;
    A. angekosa wanyama wa kumfanyia kazi shambani.
    B. angekosa pesa za kuweka katika benki.
    C. angeshindwa kabisa kulipa ushuru.
    D. angeshindwa kuanzisha kilimo chake.
4. Benki ilimpa Swara manufaa gani?
    A. Ilimpa mkopo alipokosa pesa.
    B. Ilimtunzia pesa zake.

C. Ilimpa ushahuri kuhusu kilimo.
D. Ilimsaidia kuuza mazao yake.

5. Marafiki wanaozungumziwa katika ufahamu huu walikuwa na jumla ya watoto wangapi?
   A. 6
   B. 11
   C. 5
   D. 4
6. Swara alikuwa mzalendo kwa kuwa; A. aliipenda sana nchi yake.
   B. aliwapa wenzake ajira.
   C. alilipa ushuru kutokana na mapato.
   D. alikuwa rafiki wa Mbweha.
7. Kifungu hiki kinaeleza umuhimu wa mambo yafuatayo **isipokuwa**;
   A. kilimo
   B. biashara
   C. ufugaji
   D. elimu
8. Maneno '**Swara na Mbweha walipendana kama chanda na pete**' ni mfano wa;
   A. tashbihi ya umbo
   B. tashbihi ya tabia  C. istiara ya umbo
   D. nahau ya upendo

***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>***

Kijiji cha Ingusi kinapatikana kati ya masoko manne. Soko la Butere hujulikana sana kwa ununuzi wa mifugo kama vile mbuzi, nguruwe, kondoo na mbuzi. Katika soko lilo hilo, kunapatikana nguo za watu wa kike na kiume, watoto kwa watu wazima. Wanaotaka kununua viungo vya upishi kama vile mafuta, vitunguu, nyanya na chumvi nao wanaweza kununua katika soko hilo. Upande mwingine, utapata soko la Mumias. Kwenye soko hilo, unaweza ukanunua mifugo mbalimbali. Aidha, unaweza ukununua jezi za timu mbalimbali kama vile Gor Mahia, AFC Leopards, Manchester United, PSG na kadhalika. Vifaa mbalimbali vinavyotumika nyumbani kama vile sufuria, vikombe, mabeseni, vijiko na visu viliuzwa sokoni hapo. Nyanya, mafuta ya kupikia, vitunguu, mdalasini na bizari pia huweza kupatikana katika soko hilo.

Soko la Imanga nalo linapatikana karibu na kijiji cha Ingusi. Kwenye soko hilo la Imanga, wanunuzi hupata bidhaa nyingi zisizopatikana katika masoko hayo mengine. Kile kinachopatikana kwenye soko hilo na lile la Butere ni viungo vya kupikia. Soko la Ugunja linafahamika kwa bidhaa moja muhimu sana. Wakazi wa Ingusi huenda kwenye soko la Ugunja kwa sababu ya kununua samaki mbalimbali kama vile mkunga, kipepeo, pweza na kambare.

9. Ni nini kinachopatikana katika masoko matatu?
    A. vifaa vya kupikia
    B. viungo vya kupikia
    C. jezi za kuchezea
    D. mavazi mbalimbali
10. Waliotaka kununua mifugo wangetembelea masoko gani?
    A. Butere na Imanga
    B. Butere na Mumias
    C. Mumias na Imanga
    D. Ugunja na Butere
11. Soko lipi linalojulikana kwa bidhaa za aina moja pekee?
    A. Mumias
    B. Butere
    C. Imanga
    D. Ugunja
12. Kifungu kimetaja samaki wa aina ngapi?
    A. 4
    B. 3
    C. 5
    D. 6

***<u>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>*** ***(Kando ya barabara, Farida anakutana na Juma akiwa amebeba jembe.)***

**Farida:** Hujambo Juma?
**Juma :** Sijambo Farida. Umeadimika sana. (***Wanashikana mikono wakitabasamu.***)
**Farida:** Si sana. Je, unatoka wapi na jembe?
**Juma :** Mimi pamoja na vijana wenzangu tumekuwa **tukichanga bia** shambani. Farida

**Farida:** Hewaa! Jambo zuri sana. Nami ninatoka katika shughuli za kufanya mazoezi. Tangu nilipokuwa na umri mdogo, nimekuwa nikifanya mazoezi mara kwa mara. Kesho nitahamia kule Marekani, nimechaguliwa kuwa mchezaji katika timu moja ya kandanda.
**Juma :** Hongera. Uamuzi huo ni wa busara mwenzangu. Ningependa nifike nyumbani ili nipumzike kiasi.
**Farida:** Buriani Juma.
**Juma :** Buriani dawa. (***Wanapigana pambaja kisha kila mmoja anaondoka.***

13. Ni kweli kuwa Farida;
    A. anapenda masomo.
    B. anapenda kilimo.
    C. anapenda afya yake.
    D. anapenda nchi yake.
14. Nahau 'tukichanga bia' ina maana gani jinsi ilivyotumika katika mazungumzo?
    A. tukilima
    B. tukifanya bidii
    C. tukishirikiana
    D. tukizungumza
15. Ni kweli kuwa Farida na Juma;
    A. wangeonana tena shule zikifungwa.
    B. hawakutarajia kuonana hivi karibuni.
    C. walisomea katika shule moja.
    D. walikuwa marafiki kwa muda mrefu.

***<u>Chagua jibu lifaalo ili kujazia nafasi zilizoachwa.</u>***

Kenya ni nchi __**16**__ makabila mengi. Makabila haya yanapatikana nchini__**17**__. __**18**__ tuishi vizuri, tunafaa kuwa na amani na umoja kati __**19**__. Umoja huo utatuwezesha kupiga hatua za kimandeleo na __**20**__ uchumi wetu.

| | **A** | **B** | **C** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | yenyewe | lenye | yenye | lenyewe |
| **17.** | mote | pote | yote | kote |
| **18.** | Ikiwa | Ila | Ili | Lakini |

Revision Material: CBC Resources.co.ke | Enovate CBC App | Highschool.co.ke

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **19.** | yetu | yenu | yao | yangu |
| **20.** | kuijenga | kuujenga | kuyajenga | kumjenga |

21. Chagua sentensi iliyo sahihi.
    A. Mgeni mwenye amewasili ni huyu.
    B. Hii kalamu ilinunuliwa jana.
    C. Mtoto mgani mwenye mikono safi?
    D. Walitupa kalamu nzuri tukafurahi.
22. Ishara gani kwenye tarakilishi ambayo huonyesha **chapa koza**?
    A. I
    B. B
    C. X
    D. U
23. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mistari. <u>Wewe</u> una kalamu <u>ambayo</u> ni nzuri.
    A. kivumishi, kivumishi, kiwakilishi
    B. kiwakilishi, kivumishi, kivumishi
    C. kiwakilishi, kiwakilishi, kivumishi
    D. kivumishi, kielezi, kivumishi
24. Kipande cha kwanza cha mshororo wa shairi huitwaje?
    A. ukwapi
    B. utao
    C. vina
    D. mizani
25. Tambua umoja wa;
    **Makazi yao yamezungushiwa nyua nzuri.**
    A. Makazi yao yamezungushiwa ua mzuri.
    B. Makazi yake yamezungushiwa ua mzuri.
    C. Kazi yake imezungushiwa ua mzuri.
    D. Makazi yake yamezungushiwa ua zuri.
26. Kiungo cha mwili ambacho huhifadhi mkojo tumboni huitwa __________________________.
    A. figo
    B. pafu
    C. kibofu
    D. moyo

27. Chagua ukubwa wa;

**Mzee huyo amebeba ndoo iliyokuwa chini ya mti.**

A. Jizee hilo limebeba jidoo lililokuwa chini ya jiti.
B. Kizee hicho kimebeba kidoo lilichokuwa chini ya kijiti.
C. Zee huyo limebeba doo lililokuwa chini ya jiti.
D. Zee hilo limebeba doo lililokuwa chini ya jiti.

28. Soma ni kwa 'somewa' kama vile nyoa ni kwa ____________________________.

A. nyoewa
B. nyoana
C. nyolewa
D. nyoleka

29. Nomino gani inayopatikana katika ngeli ya U-U kati ya nomino zifuatazo?

A. ubua
B. ukuta
C. unga
D. mkono

30. Alama gani ya kuakifisha ambayo hutumika kuanzishia orodha?

A. koloni
B. ritifaa
C. hisi
D. koma